



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli  
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222  
Faksi: +255 22 2111281  
Barua Pepe: [chragg@chragg.go.tz](mailto:chragg@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

---

Februari 1,2017

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **Tamko la THBUB kukemea vitendo vinavyokiuka utawala Bora katika utekelezaji wa majukumu ya viongozi wa wilaya.**

---

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeshitushwa na taarifa ya matukio yanayohusisha wananchi wa kijiji cha Mlongia, Wilaya ya Chemba, Mkoani Dodoma kumpiga mawe ndugu Simon Odunga, Mkuu wa Wilaya hiyo ambaye anatumiziwa kummilikisha mwekezaji ardhi ya wanakijiji hao bila ya kufuata taratibu.

Kulingana na taarifa za vyombo vya habari tukio la kupigwa mawe Mkuu wa Wilaya, lilifuatiwa na agizo la kukamatwa wanakijiji kwa amri ya Mkuu wa Wilaya. Matukio yote haya hayaendani na dhana ya utawala wa Sheria na Utawala Bora.

Aidha, Tume inawakumbusha Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutumia madaraka yao ya ulinzi wa amani kwa kufuata Sheria ya Tawala za Mikoa, Sura 97 ya Sheria za Tanzania 2002, hususan vifungu namba 7 na 15, ambavyo vinawataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanapoamuru mtu akamatwe, kufuata taratibu ikiwemo ulazima wa kutoa sababu za kumkamata mtu kwa maandishi, mbele ya Hakimu ndani ya masaa 48, au mtu huyo aachiwe huru.

Vifungu namba 7(9) na 15 (9) vya Sheria hiyo vinatamka kwamba Mkuu wa Mkoa na Wilaya au mtu mwingine yeyote, asipozingatia matakwa ya sheria hiyo, atakuwa ametenda kosa la jinai.

Ifahamike kwamba Ibara ya 130(1)(c) na (f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaipa Tume mamlaka ya kufuatilia uvunjifu wa haki za binadamu na utawala bora, na utekelezaji wa madaraka ya kazi au majukumu ya mtu au taasisi yeyote wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wilaya, iwapo utekelezaji wa majukumu yao **utakiuka** madaraka yao.

Kufuatia tukio lilitokea Kijiji cha Mlongia, Wilaya ya Chemba, Tume inapenda kushauri yafuatayo;

1. Wananchi wazingatie sheria na taratibu za nchi katika kutatua kero zao za kila siku, kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kuleta amani na utulivu na kuondoa migogoro isiyo ya lazima.
2. Wakuu wa Mikoa na Wilaya wazingatie sheria husika, kanuni na taratibu zilizowekwa wanapoagiza wananchi kukamatwa. Kwa kufanya hivyo utawala wa Sheria utadumishwa.
3. Dhana ya Utawala Bora inamtaka kila mtu kuheshimu Sheria, na inawataka viongozi kutotumia madaraka yao vibaya. Hivyo basi kwa kuwa viongozi wanawajibu wa kusimamia sheria, wanatakiwa kujua kwamba na wao pia wako chini ya sheria na wanapaswa kufuata sheria za nchi, na si vinginevyo.

Imetolewa na:

  
Mhe. Bahame Tom Nyanduga  
**Mwenyekiti**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Februari 1, 2017